For more visit: eazyarabic.com

**KCSE 2022 PAPER 2**

## 5.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

1. **UFAHAMU**

(a)

(i) Aliandamana na wanafunzi ziarani.
(ii) Aliwaelekeza wanafunzi kwenye sehemu mbalimbali za maonyesho.
(iii) Alimtia moyo Lena.
(iv) Aliwashauri wanafunzi.

**Hoja 2 x 1 = 2**

(b)

(i) uwepo wa vipepeo na nyuki bustanini
(ii) vipepeo kusambaza mbegu na mimea kunawiri
(iii) wadudu kuwa lishe kwa binadamu
(iv) binadamu kurina asali kutoka kwa nyuki
(v) watalii kuzuru kijiji cha Faidi (Kijiji cha Vipepeo)
(vi) kijiji kunufaika kutokana na ada iliyotozwa

**Hoja 5 x 1 = 5**

(c)

(i) Kupata wazo/ kuwa na wazo la kuanzisha mradi.
(ii) Kuanzisha mradi wa vipepeo.
(iii) Kuendeleza mradi – kuwalea/ kuwatunza vipepeo.
(iv) Kunufaika kutokana na ada – kufanyiwa kwa utafiti, kufadhiliwa.
(v) Kijiji kupata umaarufu.
(vi) Miundomsingi kuimarika.

**Hoja 3 x 1 = 3**

(d)

(i) Ni kiongozi wa chama cha wanamazingira.
(ii) Alimuuliza mwalimu swali.
(iii) Aliwarai wenzake kuhusu mradi wa ufugaji wa vipepeo.
(iv) Alijibu maswali kwenye runinga.

**Hoja 2 x 1 = 2**

(e)

(i) mpangilio/ utaratibu/ mfululizo wa shughuli/ mchakacho/ mfuatano/ njia ya kufanya jambo
(ii) haraka, wepesi

**Hoja 2 x 1 = 2**

(f)

(i) Ufugaji/ uhifadhi wa vipepeo
(ii) Vipepeo
(iii) Mradi wa vipepeo

**Hoja 1 x 1 = 1**

For more visit: eazyarabic.com

2. **UFUPISHO**

(a)

(i) Matarajio ya vijana ni kupata ajira.
(ii) Vijana wachache wanaohitimu hupata ajira.
(iii) Kuna tatizo la uhaba wa ajira nchini na ulimwenguni kote.
(iv) Serikali imewekeza katika maswala ya vijana.
(v) Tatizo la ajira kwa vijana linahitaji suluhisho la kudumu.
(vi) Maarifa aliyo nayo mtu ndio huchangia kuajiriwa kwake.
(vii) Wapo wanaokosa ujuzi na maarifa kwa sababu ya kutokuwa makini.
(viii) Vijana wanakosa ajira kwa kutokamilisha kozi fulani.
(ix) Vijana wanakosa ajira kwa kuwa hawakupata ujuzi wa kuwawezesha kuajiriwa.
(x) Vijana kuachishwa kazi kwa kukosa kuwajibika.
(xi) Baadhi ya vijana huwa na mazoea ya kuchagua kazi.
(xii) Vijana kutamani utajiri wa haraka bila kujali njia watakazotumia kupata utajiri huo.
(xiii) Vijana kutegemea walezi kwa kila kitu.
(xiv) Vijana kuchelea kuajiriwa kwa kuhofia kukosa muda wa kujumuika na wenzao.
(xv) Kuwepo kwa vijana wanaoshinikizwa na wenzao kukataa ajira.

**Hoja 8 x 1 = 8**

(b)

(i) Pana haja ya kuwa na ajira zenye staha na manufaa kwa wote.
(ii) Ukosefu wa ajira umewafanya vijana kushiriki katika shughuli zisizokuwa na thamani.
(iii) Wapo vijana wanaofanya kazi zisizoambatana na maarifa waliyo nayo.
(iv) Vijana hufanya kazi katika mazingira magumu na yenye kuhatarisha maisha yao.
(v) Vijana hufanya kazi kwa muda mrefu na kuathiri afya yao.
(vi) Kuna vijana waliopokea malipo duni.
(vii) Vijana kushawishika kwa wepesi na kushiriki katika maovu.
(viii) Vijana huwa na malimbikizi ya madeni.
(ix) Ukosefu wa ajira huchangia kuwepo kwa mitafaruku katika familia.
(x) Kuna uwezekano wa kudidimia na kusahaulika kwa maarifa.
(xi) Vijana huchushwa na kuchoshwa na makali ya maisha.
(xii) Vijana hujitenga na wanajamii.
(xiii) Vijana hushiriki katika matumizi ya dawa za kulevya na unywaji wa pombe kupindukia ili kujiliwaza.

**Hoja 6x 1 = alama 6**

**Mtiririko alama 1**

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) (i) / i / ½ / **0**
(ii) / o / ½/ 0

(b) (i) bi-ngi-ri'-a au bi-ngi-<u>ri</u>-a ½ / 0
(ii) wa-li-mwe'-ngu au wa-li-<u>mwe</u>-ngu ½ / 0

(c) (i) a – nafsi ya tatu/ mtenda/ngeli/ kiambishi cha kiima/ umoja/ idadi
na – wakati uliopo
vyo – kirejeshi/ namna/ jinsi
jeng – mzizi
a – kiishio/ kauli ya kutenda **1/ 0**

For more visit: eazyarabic.com

(ii) m – kiambishi ngeli/ umoja/ mtenda/ idadi/ kiima
fariji – mzizi **1/ 0**

(d) yupo – kitenzi kishirikishi **1/ 0**
anapalilia – kitenzi halisi **1/ 0**

(e) Mwashi alijenga jumba la kifahari la kupendeza. **1/ 0**

(f) Barabara zote zilikarabatiwa na wahandisi baada ya mafuriko.

Barabara zote zilikarabatiwa baada ya mafuriko na wahandisi. **1/ 0**

(g) Serikali imebuni mikakati ya kukabiliana na **wingu la nzige** wanaovamia/ linalovamia mashamba. **1/ 0**

(h) Sentensi ibainishe mojawapo ya matumizi yafuatayo:
(i) Kuleta maana ya *ama/au.*
- Kalamu/karatasi inahitajika.

(ii) Kuonyesha maneno yenye maana sawa.
- Watalii waliona ndovu/ tembo mbugani.

(iii) Katika kuandika akisami.
- $\frac{1}{7}$

**1/ 0**

(i) Wanariadha hawajaenda uwanjani kufanya mazoezi.
**1/ 0**

(j) (i) Watalii walifika katika mbuga ya Tsavo ambako waliwaona wanyamapori. **1/0**
(ii) Mkurugenzi aliwapa ushauri wafanyakazi watie/ kutia bidii kazini.
Mkurugenzi alitoa ushauri kwa wafanyakazi watie/ kutia bidii kazini. **2/0**

(k) KN – Vipepeo wale weupe
– Mvua ya masika
KT – Wanaashiria mvua ya masika inayotarajiwa mwakani
– inayotarajiwa mwakani
KV – wale weupe
**4 x ½ = 2**

(l) Wakongwe – yambwa tendewa/ kitondo
nyumba – yambwa tendwa/ kipozi
mawe- yambwa ala/ kitumizi
Majibu yoyote mawili **2x1= 2**
kwa mawe – chagizo **1/0**

(m) Huduma za afya zinapoboreshwa viwango vya maambukizi hupungua.
au
Huduma za afya ziboreshwapo viwango vya maambukizi hupungua.
**2/0**

(n) Chifu aliwaambia wafanyabiashara kwamba/ kuwa watunza mazingira wangenadhifisha soko lao siku ambayo ingefuata.

**2/0**

(o) (i) Kuonyesha mfuatano wa matukio au vitendo, kwa mfano:
Mkulima alipanda mbegu, a**ka**pakilia, a**ka**vuna, a**ka**uza.
(ii) Kuonyesha kitendo kimoja kinasababishwa na kingine, kwa mfano:
Alitia bidii masomoni a**ka**tuzwa.
(iii) Kuonyesha nia au matarajio ya kufanyika kwa jambo fulani, kwa mfano: Nitakutuma sokoni u**ka**ninunulie mboga.
(iv) Kuleta wazo la kuamrisha kwa mfano:
**Ka**ondoe uchafu wote uani! (amri)
(v) Kuleta wazo la rai, kwa mfano:
**Ka**mhudumie mteja wetu. (rai)
(vi) Katika usemi halisi, kwa mfano:
"Nitakuja kesho." Mama a**ka**sema.

**2 x 1 = 2**

(p) (i) bendera – I-ZI **1/ 0**
(ii) ujana – U-U au U **1/0**

(q) Vigoma/ vijigoma hivyo vimetengenezwa kwa vigozi/ vijigozi laini.
au
Vigoma/ vijigoma hivyo vimetengenezwa kwa kigozi/ vijigozi laini.

**2/ 0**

(r) Watahiniwa watumie vihisishi kama vile: kumbe!, Lo!, Eti!, Ati!, Salaala!, Salaale!, Aa!, Aha!, Hivyo!, Afanalek!, Mungu wangu!

**1/0**

(s) KN(N + $\overline{S}$ ) + KT(T) + KN (N + V)
Madereva waliopata mafunzo wamepokea leseni mpya.

**3/ 0**

(t) (i) Jena hakufuata ushauri wa mwelekezi wake hivyo hakufaulu.
(ii) Jena hana nafasi ya kufuata ushauri wa mwelekezi wake ili afaulu kwa sababu kitendo kimefanyika.

**2 x 1 = 2**

(u) busara **1/0**
ombi/ bembeleza/nasihi/ sairi/ rai **1/0**

(v) Watahiniwa watunge sentensi **moja tu** kubainisha maana **mbili** za neno **hema**.
hema - kibanda cha chadarua
hema- tokwa na pumzi kwa nguvu
Kwa mfano: Wanariadha waliokimbia na kuhema walipumzika ndani ya hema.

**2/ 0**

(w) Mchagua jembe si mkulima. **1/ 0**

For more visit: eazyarabic.com

4. **ISIMUJAMII**

**(a)** Biashara/ viwandani/ sokoni

(i) Matumizi ya msamiati maalum wa biashara. K.m. wateja, bidhaa

(ii) Matumizi ya lugha ya kuamrisha. K.m. Kazi ianze mara Moja!

**Kubainisha alama 1**
**Mfano alama 1**

**(b)**

(i) Matumizi ya lugha ya unyenyekevu. Kwa Mfano, wafanyikazi wanapozungumza na meneja.

(ii) Matumizi ya kauli fupifupi/ lugha ya mkato. Kwa mfano, kazi ianze mara moja.

(iii) Matumizi ya misimu kutegemea shughuli katika biashara husika. Kwa mfano, tunza wira.

(iv) Kuchanganya ndimi/ msimbo/ lugha.

(v) Kuhamisha msimbo/ kubadili msimbo/ kugeuza msimbo.

(vi) Matumizi ya lugha rasmi hususan mikutanoni.

(vii) Kurudiwarudiwa kwa kauli/ matumizi ya lugha yenye uradidi.

(viii) Matumizi ya lugha isiyo sanifu.

(ix) Matumizi ya lugha ya ishara ili kupunguza mawasiliano ya mazungumzo.

(x) Matumizi ya lafudhi.

(xi) Matumizi ya maswali na majibu/ udadisi.

(xii) Matumizi ya maswali ya balagha.

(xiii) Lugha ya utani.

(xiv) Maelezo/ matumizi ya sentensi ndefu.

(xv) Matumizi ya tamathali za usemi.

**8 x 1**
**Kutaja - ½**
**Mfano - ½**